Padre Pancratius Pfeiffer SDS

Mtume – Kiongozi – Mtu wa amani

Sala ya Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Miaka 75 tangu Kifo chake [1]

1. Utangulizi:

Karibuni nyote kwa wakati huu wa sala za pamoja ambazo kwazo twataka kuheshimu kumbukumbu ya miaka 75 ya kifo cha mpendwa wetu Padre Pancratius Pfeiffer (1945-2020). Pamoja na Familia yetu yote ya Kisalvatorian tunapenda kumtolea Mungu shukrani kwa ushuhuda wake uliotukuka wa maisha ya wakf kama Msalvatorian mtume, kiongozi na chombo cha amani. Katika historia ya maisha ya Pancratius tunapata ushuhuda wa uaminifu wa nini maana ya kuishi kwa undani utume wa karama ya Padre Fransis Jordan.

- Uje Roho Mtakatifu …
- Wimbo: *Salvator mundi (au wimbo mwingine)*

2. Sala ya Mwanzo:

Mungu wa fadhili na upendo, tunapokumbuka na kuheshimu maisha ya Padre Pancratius Pfeiffer katika maadhimisho ya miaka 75 ya kifo chake, tusaidie kutambua na kujazwa roho ya neema ya ajabu ya huduma kwa wote, na hasa wakati huu.
Kama ambavyo tunakabiliwa na changamoto nyingi za kiulimwengu, fungua mioyo, akili na roho zetu ili kwa pamoja tuweze kusonga mbele kwa ujasiri kama mwili mmoja wa Kristo, Mungu Mwokozi wetu – ili kwa shukrani tubarikiwe, tumegwe na kugawanywa kwa wengine kwa faida ya wote. Tunaomba hayo katika jina lako takatifu. Amina.

3. Reading from Titus 2:11-14 and 3:4-7

- *Katika tukio la maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa Shirika, Padre Pancratius Pfeiffer, kama Mkuu wa Shirika, aliamuru aya za Barua kwa Tito 2:11-13 kuandikwa kwenye kuta za kikanisa cha nyumbamama. Maandishi haya, "Fadhili na upendo wa*

[1] Huduma hii ya Sala imetayarishwa na Halmashauri Kuu ya Shirika la Wasalvatorian. Roma, Mei 2020

Mungu umedhihirishwa kwa wanadamu katika Mungu Mwokozi wetu", yaliwazwa kabla na Mwanzishi wetu, lakini yalifanywa maarufu na Padre Pfeiffer.

Msomaji: "Maana neema ya Mungu imefunuliwa, kwa ajili ya wokovu wa watu wote, nayo yatufunza kukataa ubaya na tamaa za kidunia; ili tuwe na kiasi, tuishi maisha adili na ya kumcha Mungu, katika ulimwengu huu wa sasa, tukiwa tunangojea siku ile ya kheri tunayoitumainia, wakati utakapotokea utukufu wa Mungu Mkuu na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Yeye alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu ili atukomboe kutoka katika uovu wote na kutufanya watu safi walio wake yeye mwenyewe, watu tulio na hamu ya kutenda mema … Lakini wakati wema na upendo wa Mungu, Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa si kwa sababu ya jambo lolote jema tulilotenda sisi, bali kwa sababu ya huruma yake, kwa njia ya Roho Mtakatifu anayetujalia tuzaliwe upya na kuwa na maisha mapya kwa kutuosha kwa maji. Mungu alitumiminia Roho Mtakatifu bila kipimo kwa njia ya Yesu Kristo, Mwokozi wetu, ili kwa neema yake tupate kuhesabiwa haki na kuwa warithi katika tumaini la uzima wa milele." *Neno la Bwana*

Tafakari ya Kimya

Ni kwa namna gani tunatoa ushuhuda juu ya ukarimu wa upendo wa Mungu na fadhili zake leo?

4. Ushuhuda juu ya Maisha ya Padre Pancratius Pfeiffer:

4.1 - Mtume Msalvatorian wa Mfano

Padre Pancratius Pfeiffer aliingia Shirikani akiwa na umri wa miaka kumi na sita. Mara tu baada ya kupadrishwa, tokana na hekima yake, moyo wa huruma, na majitoleo yake ya kitume, aliweza kuhusishwa kwenye majukumu ya kiuongozi ya Shirika. Kama mkono wa kuume wa Padre Jordan, vilevile alikuwa mhimiri wa mawasiliano kwa maofisa wa ngazi za juu wa Vatikano kwa miaka mingi.

a. "Lakini ninamshukuru Bwana mwema kwa kumfahamu binafsi Mheshimiwa sana Baba Mkuu. Katika matukio machache nimeweza kufahamu baadhi ya tunu zake bora. Nimeona na kung'amua ukuu wake adhimu: moyo wake mkuu wa kusaidia daima; moyo mwema wenye kupendeza na usio na makuu; wenye furaha na wa kiuhalisia, nao iliungana na nguvu yake isiyo ya kawaida." (Sista M. Regis, *Mama Mkuu wa Shirika la Kitume la Watumishi wa Roho Mtakatifu)*

b. "Ni zawadi nzuri kiasi gani ambayo Bwana atampatia baada ya maisha yake yaliyojaa kazi na utakatifu muda wote! Nyumba yetu ndogo ilipata heshima ya kuwa nae kama mlezi wa kiroho kwa zaidi ya miaka 40 … wasichana wetu, ambao kila asubuhi walisubiri neno jema toka kwake na mara nyingi tafakari ambayo ilitoa ujumbe wa furaha yenye afya. Na kwa Masista wetu, aliwapatia mfano wa utaua, wa tafakari, kujikana, wa uaminifu kwa utume wetu … (Sista Margerita Defasques, *Mabint wa Upendo)*

c. “Padre Pancratius daima alitujenga na kutuimarisha kwa mfano wa maisha yake angavu. Daima alikuwa kwenye hali ya uchangamfu licha ya hofu zake zisizo na idadi. Alikuwa na busara ya pekee, upendo usio na mipaka, na daima mwenye tabasamu. Ni mara ngapi wakati huu wa vita tumeshangazwa na utuliva wake na roho yake ya sadaka. Mara nyingi baada ya Misa, tuliweza kumwona akiwafariji au kuwatia moyo watu wa hali zote waliokuwa wakimsubiri ili kutulizwa mahangaiko yao. Baada ya Misa, Padre Pancratius anaweza kutumia muda kwenye piano kuimba Zaburi au tenzi kwa Mama yetu Bikira Maria. Anaweza kucheza, kuimba na kucheka, akisema kwamba huu ulikuwa ni muda wa kujipumzisha kwa siku yake.” (Sista Margarita Defasques, *Mabint wa Upendo*)

- Ukimya mfupi…
- Wimbo: Laudate omnes gentes *(au wimbo mwingine)*



4.2 – Kiongozi Msalvatorian

Wakati wa Mkutano Mkuu wa III wa Shirika, Padre Pancratius Pfeiffer akiwa na umri wa miaka arobaini na tatu alikuchaguliwa kuwa Mkuu wa Shirika wa kwanza kumrithi Baba Mwanzishi. Alipokea jukumu hilo kwa uimara na ushujaa kwa miaka thelathini. Aliliongoza Shirika kusonga mbele na katika mafanikio ya baadaye.

a. “Shirika letu lilibakia na linabakia lenye shukrani kubwa kwake Marehemu Mheshimiwa sana Baba Mkuu kwa msaada na ushauri wake mwema, hasa wakati wa miongo iliyopita. Mimi binafsi nakumbuka kwa shukrani masaa mengi ya majadiliano niliyofanya na yeye, na ambayo kwayo nilirudi tena na tena nikiwa nimeimarika nafsini na kuwa na ari ya kufanya kazi yangu” (Padre Joseph Grendel SVD, Mkuu wa Shirika la SVD)

b. “Padre Pancratius Pfeiffer alijaliwa tunu bora za kidiplomasia, ukiachilia mbali werevu ambao daima haukuwekewa mashaka. Nguvu yenye kupenya ya unyenyekevu wa hotuba yake ulishangaza. Alijua kila kitu lakini aliongea yale muhimu tu. Kumbukumbu yake imara ilimruhusu kuwa wa kisasa na mwenye kwenda na wakati; mtu mwenye upeo wa juu usiyopingana na maisha yake ya kiroho.” (*Leone Gessi, Mwandishi wa Habari wa The Messenger of Rome)*

c. Hatuwezi kumsahau katika sala zetu huyu mtawa, ndugu na Mkuu wa Shirika mashuhuri, na tukumbuke kauli-mbiu yake: “Shirika litaimarika kwa kiwango ambacho kila mmoja atatimiza wajibu wake.” Mifano angavu mitatu: Mstahiki Baba Mwanzishi, Padre Bonaventura Luthen na Padre Pancratius Pfeiffer na wawe waombezi wetu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu ili kwamba Shirika letu liweze kupata tena kiongozi ambaye atafuata nyayo za hawa watu watatu wakuu na watakatifu.” (Padre Bonaventura Schweitzer SDS, *Mkuu wa Provinsi ya Wasalvatorian ya Ujerumani Magharibi)*

- Ukimya mfupi…

- **Wimbo:** Adoramus Te Domine *(au wimbo mwingine)*



4.3 - Msalvatorian Mtu wa Amani

Wakati wa Vita vya Pili vya Dunia alipewa jina la "Malaika wa Roma" tokana na kuokoa maisha ya watu wengi hasa Wayahudi. Alikuwa ni kiungo muhimu kati ya Papa Pius XII na majenerali wa Kijerumani. Alifariki akiwa na umri wa miaka sabini na tatu siku ya tarehe 12 Mei 1945, baada ya kugongwa na gari.

a. "Nilikuwa rafiki na mstaajabivu wa Padre Pancratius Pfeiffer ambaye nilithamini ubora wa hali ya juu wa moyo wake na maisha yake ya kiroho. Nilimuelewa wakati wa janga na masaa magumu. Ninaomboleza kifo chake cha ghafla na cha huzuni, na ninatuma salamu zangu za rambirambi za dhati kwa jumuiya yake." (**Ivanoe Bonomi**, Waziri Mkuu wa Serikali ya Italia)

b. "Kwa hakika, nilipomuona Padre Pancratius akinikaribia gerezani, nilivutwa sana moyoni. Baada ya mshtuko wa mara ya kwanza ambao ulinipata nilipomuona mbele yangu na macho yake ya bluu, na tabasamu lake angavu la matumaini, nilielewa kwamba alikuwa mhamasishaji wa ukombozi na wema. Ninastahili maisha yangu yaokolewe kwa Maongozi ya Mungu, kwa Padre Pfeiffer na kwa marafiki zangu. Katika kijarida cha kumbukumbu, nilisoma dondoo nzuri sana kuhusu Wasalvatorian, "Tunaamini katika Maongozi ya Mungu, katika kukabiliana na matatizo ya wakati huu, kila mahali na kwa kila kipindi cha kihistoria." Nilikuwa na fursa ya kuonja ni kwa namna gani wazo lile lilikuwa halisia wakati ule wa kipindi cha historia ya kutisha, wakati wa miezi tisa ya uvamizi wa Wajerumani dhidi ya mji wa Roma." (**Giuliano Vassalli,** Seneta Muitaliano)

c. "Nikajikuta niko mbele ya mtu wa kawaida, mwenye kufikika na ndugu-mdogo mwenye tabasamu, na wala si mbele ya mwenye makuu kama nilivyofikiri akilini mwangu. Mara tu baada ya kusikia juu ya hali yangu, aliniambia, "Nitafanya kila ninachoweza kwa ajili ya mwanao." Nilionja utayari wake wa kusaidia na namna alivyosaidia kwa mapendo ya Kristo. Na nilimbariki toka ndani ya moyo wangu uliovunjika." (Clara Mattei Friedmann, mama wa mfungwa wa kivita)

- Ukimya mfupi…
- **Wimbo:** Ubi Caritas *(au wimbo mwingine)*

5. Sala za Waamini

Tukiwa na shukrani kwa ushuhuda wa Kisalvatorian wa Padre Pancratius Pfeiffer, sasa na tuinue sala zetu tukitumaini kuwa sisi sote ni wana wapendwa wa Mungu:

a. Tuombe kwa ajili ya Familia yote ya Kisalavatorian, ili kwamba mfano wa utume wa Padre Pancratius Pfeiffer utuhimize kuishi wito wetu wa kuwa mitume wa leo kwa furaha, shauku na uaminifu.

Baba Yetu … Salaam Maria … Atukuzwe …

b. Tuombe kwa ajili ya Wasalvatorian wote walioitwa kushika mamlaka kati yetu ili waweze kufuata mfano wa Padre Pancratius Pfeiffer katika kueneza utume wetu kwa wema na uthabiti duniani kote.

Baba Yetu … Salaam Maria … Atukuzwe …

c. Tuwaombee watu wote waliojidhatiti kulinda uadilifu wa maisha na wanaotafuta kutenda haki na kukuza amani kadiri ya tunu za Injili, kama tulivyooneshwa mfano na Padre Pancratius Pfeiffer.

Baba Yetu … Salaam Maria … Atukuzwe …

a. Tuombee … (nia zingine)

Baba Yetu … Salaam Maria … Atukuzwe …

Mungu Mwenyezi, tunatoa maombi haya yote tukitumaini kuwa unatusikia. Tunaamini kuwa utatutimizia mahitaji yetu, na wala siyo matakwa yetu, kwa maombezi ya Mstahiki Padre Jordan, mshauri na baba wa kiroho wa Padre Pancratius Pfeiffer. Amina.

6. Closing Prayer:
Mungu Mwenyezi, tunatoa maombi haya yote tukitumaini kuwa unatusikia. Tunaamini kuwa utatutimizia mahitaji yetu, na wala siyo matakwa yetu, kwa maombezi ya Mstahiki Padre Jordan, mshauri na baba wa kiroho wa Padre Pancratius Pfeiffer. Amina.

- **Wimbo wa Mwisho:** Regina coeli *(au wimbo mwingine)*